



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, akizungumza na wakulima na wafugaji katika Kijiji cha Njiwa kilichopo Wilaya ya Malinyi mkoani Morogoro juzi kuhusu taarifa ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ya uwepo wa vipindi virefu vya ukavu vilivyojitokeza katika kipindi cha Mwezi Machi na Aprili mwaka 2022 unaotishia upungufu wa malisho ya mifugo na maji. NA MPIGAPICHA WETU.

Upatikanaji chanjo ya sato kuongeza mavuno

Na Happy Mollel, Simiyu

TUME ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) imesema inaendelea na utafiti wa chanjo ya samaki aina ya sato.

Imesema kupatikana kwa chanjo hiyo kutaongeza mavuno ya samaki na hivyo kuongeza tija na kipato.

Mratibu wa Utafiti kutoka Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia nchini, Dk Beatrice Tarimo alisema hayo wakati wa kikao kilichojadili masuala muhimu ya utafiti wa mazao ya kilimo, mifugo na viumbe hai vya majini.

Katika kikao hicho kilichofanyika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Mjini Bariadi, alisema bado utafiti unaendelea na kwamba ukikamilika utasaidia sana kuongeza soko la biashara ya uzalishaji wenye tija kwa taifa na ambao utamnufaisha kila mtu.

Hata hivyo, alisema teknolojia hiyo ya chanjo ya samaki ni lazima ikidhi vigezo vya nchi kabla ya kuanza kutumika.

"Lakini baada ya kufanya utafiti kuna mamlaka ambazo zinahusika kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, kile kilichotengenezwa ni sahihi na kinaweza kutumika," alisema Dk Beatrice.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Dk Yahaya Nawanda, amewataka wataalamu wote mkoani hapa kufanya kazi zenye matokeo chanya, huku Ofisi ya Makamu wa Rai- (Mazingira) ikihimiza matumizi sahihi ya sheria za nchi.

"Nichukue nafasi hiji kuwaagiza wataalamu wote wa kilimo, basi twendeni tukakae pamoja tutengeneze maudhui ya pamoja (ya elimu ya kitafiti), halafu tukayasambaze kwa maafisa ugari wa wilaya na wao watasambaza kwa maafisa kilimo katika ngazi ya kata na vijiji. Basi mwisho wa siku hii teknolojia ambayo leo tumejifunza iwe kurwafikia wananchi walio wengi zaidi," alisema Nawanda.